**HISTORIA YA UJASIRIAMALI**
Kwa mujibu wa mtandao wa Wikipedia ,Neno Ujasiriamali lina asili ya Kifaransa **" Entreprendre "** sawa na kutekeleza / kufanya shughuli fulani mwenyewe katika uwanja wa kibiashara katika maana rahisi ni sawa na kuanzisha biashara /shuguhuli ya kuingiza kipato.

Watu wengi wakiwemo wasomi wanamtazama mjasiriamali kama mtu **ANAYEONGOZA, ANYEPANGA** na aliye na UTAYARI juu ya hatari zozote zinazoweza kujitokezaa katika biashara / shughuli yake husika. Mbali na hayo mjasiriamali anatazamwa kama mtu anayechukua hatua pindi fursa inapojitokeza haijalishi ana nini mkononi mwake.

Mchumi mwenye asili ya Kiustralia Joseph Schumpter ameeleza dhana ya ujasariamali kuwa kutegemea mihimili ya **UGUNDUZI** na **UBUNIFU** katika Nyanja hizi (yaani kugundua na kubuni).

- Bidhaa mpya
- Njia mpya ya uzalishaji /uendeshaji
- Masoko mapya
- Mifumo mipya ya vikundi na Mashirikisho

Baada ya uhuru (1961) Serikali ya Tanzania iliamua kufuata sera ya uchumi hodhi, sera ambayo serikali inamiliki njia kuu za uzalishaji. Haikuwa ruhusa kwa mtu mmoja mmoja hasa viongozi kumiliki biashara. Sera hii iliimarishwa wakati wa azimio la Arusha.
Kutokana na utandawazi kuenea duniani, mfumo wa sera ya kipebari ulichukua nafasi kubwa duniani. Mfumo wa kibepari unasisitiza watu binafsi kumiliki na kuendesha biashara. Jukumu la Serikali ni kupanga sera na kusimamia.

Ni kipindi cha uongozi wa awamu ya tatu ,dhana ya ujasiriamali ilishika kasi sana. Viongozi wa serikali na jamii kwa ujumla walisisitiza kujiingiza katika ujasiriamali kwa maana ya kuanzisha na kuendesha biashara na serikali kwa asilimia kubwa ikajitoa katika uzalishaji. Makampuni makubwa yakaanza kushika hatamu.xviii